

MWANANCHI MEI 29

Kampuni yachangia ujenzi wa sekondari Mufindi

Lengo la kampuni hiyo ni kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya jamii kwenye maeneo ya vijijini.

Na Hakimu Mwafongo, Mufindi

KAMPUNI ya Green Resources Ltd (GRL), imetoa Sh1.5 milioni kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa shule za sekondari katika kata za Idete na Mapanda wilayani Mufindi na kata ya Uchindile iliyopo wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro.

Msaada huo ulitolewa juzi na Naibu Mkurugenzi wa GRL, Yuda Mkolo, kwa viongozi wa kata hizo, katika hafla fupi iliyofanyika kwenye ofisi za kampuni hiyo wilayani hapa.

Meneja Utumishi na Utawala wa kampuni hiyo, Aidan Chifwila, alisema fedha hizo zilitolewa na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Matuma Marangu, ambaye ni mwekezaji mkuu wa kampuni.

Alisema kata hizo zinapata Sh500,000 kila moja kwa ajili ya kuchangia ujenzi

wa shule za sekondari hizo ili kutatua tati-zo la wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi waliofaulu kukosa nafasi ya kuen-delea na masomo.

Akikabidhi msaada huo, Naibu Mku-rugenzi wa kampuni hiyo alisema kwa ki-asi kikubwa kampuni hiyo imekuwa ikichangia shughuli za kimaendeleo kati-ka kata hizo ambapo wamelima hekta 5,200 za misitu kwa kata zote.

Alisema mwaka jana kampuni hiyo il-itumia zaidi ya Sh170 milioni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zahanati zilizoko katika kata hizo na kuvisambaza ili ziweze kuwahudumia vizuri wananchi.

Alifahamisha kuwa mwaka 2005 wal-itumia zaidi ya Sh30 milioni kwa ajili ya ununuzi wa madawati na ujenzi wa madarasa matano katika Shule ya Msin-gi Ihefu, wilayani Mufindi.